


UTABIRI WA MVUA ZA *MSIMU* (NOVEMBA, 2024 – APRILI, 2025)



Kielelezo 1. Mwelekeo wa Mvua za Msimu (Novemba, 2024 hadi Aprili, 2025)

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Dondoo muhimu za mvua za *Msimu* (Novemba, 2024 – Aprili, 2025)

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (kanda ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyopo kusini mwa mkoa wa Morogoro) katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2024 hadi Aprili, 2025. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya, sekta binafsi pamoja na menejimenti za maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

a) Mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka:

- (i) Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Singida na Dodoma; kaskazini na mashariki mwa mkoa wa Lindi, na kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa. Aidha, mvua za Wastani hadi Juu ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Ruvuma, Mtwara, maeneo ya kusini na magharibi mwa mkoa wa Lindi, kusini mwa mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro.
- (ii) Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2024 katika mkoa wa Kigoma na kusambaa katika maeneo mengine yanayopata mvua za *Msimu* mwezi Novemba, 2024 na mwisho katika mkoa wa Ruvuma Disemba, 2024.
- (iii) Kipindi cha nusu ya pili ya msimu (Februari – Aprili, 2025) kinatarajiwa kuwa na mvua nyingi ikilinganishwa na nusu ya kwanza (Novemba, 2024 – Januari, 2025).

b) Athari na ushauri

- (i) Shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama ilivyo kawaida katika maeneo mengi katika mvua za Msimu 2024/2025. Hata hivyo, vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani.
- (ii) Kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kuongezeka, hali inayoweza kusababisha mafuriko, hasa katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko.
- (iii) Jamii zinazokaa katika maeneo yenye hatari ya mafuriko zinashauriwa kuchukua hatua stahiki.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

1. MWENENDO WA MVUA ZA VULI, 2024 NA MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2024 HADI APRILI, 2025)

1.1 Mwenendo wa Mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2024

Msimu wa Vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba, 2024 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia) pamoja na Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba)) utabiri wake ulitolewa tarehe 22 Agosti, 2024. Mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zilitarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, kwa maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria mvua zilitarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani. Msimu wa Vuli, 2024 ulitarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha. Aidha, mvua hizo zilitarajiwa kuanza kwa kusuasua wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2024 katika ukanda wa Ziwa Victoria na kusambaa katika maeneo mengine yanayopata mvua za Vuli kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Oktoba, 2024.

Mvua hizo zimeanza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na pwani ya kaskazini kama ilivyotabiriwa. Hata hivyo, maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki yameendelea kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu. Aidha, utabiri wa mvua za Vuli unatarajiwa kuendelea kama ulivyotabiriwa.

1.2 Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2024 hadi Aprili, 2025)

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama ilivyoielezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Singida na Dodoma; kaskazini na mashariki mwa mkoa wa Lindi, na kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa. Aidha, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Ruvuma, Mtwara, maeneo ya kusini na magharibi mwa mkoa wa Lindi, kusini mwa mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro. Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya pili ya msimu (Februari – Aprili, 2025) ikilinganishwa na nusu ya kwanza (Novemba, 2024 – Januari, 2025). Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

i. Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya kanda ya Magharibi. Mvua zimeshaanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2024 katika mkoa wa Kigoma na zinatarajiwa kusambaa katika mikoa mingine katika wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2024. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2025.

ii. Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2024 na kuisha wiki ya nne mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2025.

iii. Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):


Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mkoa wa Njombe, kusini mwa mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro; na Wastani hadi Chini ya Wastani katika mikoa ya Rukwa na Songwe pamoja na kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2024 na kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2025.

iv. Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi: (Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma):

Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara pamoja na maeneo ya kusini na magharibi mwa mkoa wa Lindi. Katika maeneo ya kaskazini na mashariki mwa mkoa wa Lindi, mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2024 kwa mikoa ya Lindi na Mtwara na wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Disemba, 2024 kwa mkoa wa Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2025 kwa mikoa ya Ruvuma na Mtwara; na wiki ya nne ya mwezi Mei, 2025 kwa mkoa wa Lindi.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)



Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2024 –Aprili, 2025) na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Msimu (1991-2020).

Angalizo 1: Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.

Angalizo 2: Mwelekeo wa mvua ulitolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha mvua za Msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika msimu wa mvua wa NDJFMA 2024/2025, joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki, hali inayoashiria uwepo wa hali La Niña hafifu. Vilevile, katika msimu wa mvua wa NDJFMA, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi wakati katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi, joto la bahari la wastani linatarajiwa hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2024 - Januari, 2025). Hali hii inatarajiwa kupunguza kasi ya msukumo wa unyevunyevu kutoka katika Bahari ya Hindi kuelekea nchini katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu. Kwa upande mwingine, joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola). Kwa ujumla, hali hii ya joto la bahari inatarajiwa kudhoofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo mengi yapatayo msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, hasa katika nusu ya kwanza ya msimu.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
 Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
 S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
 Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
 (IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Aidha, uwepo wa migandamizo midogo ya hewa katika maeneo ya Rasi ya Msumbiji na mashariki mwa kisiwa cha Madagascar unatarajiwa kuimarika hususan katika kipindi cha nusu ya pili ya msimu. Uwepo wa migandamizo hiyo midogo ya hewa katika maeneo hayo unatarajiwa kuvuta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kupitia katika baadhi ya maeneo nchini. Hali hii inatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo hususan yale yaliyopo nyanda za juu kusini-magharibi, kusini na maeneo jirani.

3. ATHARI NA USHAURI

Athari na ushauri umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika Dodoma tarehe 24 Oktoba, 2024.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Upatikanaji wa maji na hali ya unyevunyevu wa kutosha kwa shughuli za kilimo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Hata hivyo hali ya upungufu wa unyevunyevu inaweza kujitokeza hasa katika nusu ya kwanza ya msimu.

Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao kwa maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani. Aidha, wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea yanayoendana na hali ya ongezeko la unyevu kama vile ukungu yanatarajiwa kuongezeka na kuathiri mazao kama viazi mvingo, mahindi, mpunga, nyanya, ufuta na maharage. Vile vile, hali ya upungufu wa unyevunyevu unaweza pia kujitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Hali hii inaweza kupelekea athari katika ukuaji wa mazao ya kilimo.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa kuzingatia hali ya unyevu katika udongo, kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, kuhifadhi maji shambani, kuzuia mmomonyoko na upotevu wa rutuba kutokana na kutuwamisha maji kwa muda mrefu au mafuriko. Aidha, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo na kudhibiti kwa wakati magonjwa ya mimea na wadudu waharibifu ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

Wakulima wanashauriwa kutumia taarifa sahihi kutoka kwa maafisa ugani kwa kuzingatia utabiri wa wilaya husika katika kuchagua mbegu na zao sahihi kulingana na utabiri wa msimu. Aidha, wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kutumia utabiri wa siku na siku kumi ili kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa utabiri wa msimu.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

b) Mifugo na Uvuvi

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani, wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa malisho, maji na chakula cha samaki. Hata hivyo, milipuko ya magonjwa ya mifugo kama vile homa ya bonde la ufa, ugonjwa wa miguu na midomo, na kuzaliana kwa wadudu wadhurifu kunaweza kujitokeza. Upungufu wa mvua hasa katika nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2024 hadi Januari, 2025) unatarajiwa kuathiri upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo na kusababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Wafugaji wanashauriwa kuweka mipango mizuri ya matumizi na uhifadhi wa maji na vyakula vya mifugo. Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kutumia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri unaotolewa na maofisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kutokea na kunufaika na hali ya hewa inayotarajiwa.

c) Utalii na Wanyamapori

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinazotarajiwa zinaweza kusababisha uhaba wa malisho na maji kwa wanyamapori katika mbuga na mapori ya akiba na hivyo kusababisha migogoro kati ya wanyamapori na jamii jirani. Hata hivyo, mvua nyingi zinaweza kusababisha kutuama na kusambaa kwa maji na kusababisha kuhama kwa wanyamapori, hasa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Hali hii inaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa wanyama wanaofugwa kutokana na wanyamapori kuingia katika maeneo ya jamii yanayozunguka hifadhi na mapori ya akiba. Pia, hali hii inaweza kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa kutokana na kushambuliwa na wanyama pori.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika mbuga na mapori ya akiba na kujenga uelewa kwa jamii ili kuchukua hatua stahiki kutokana na athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo basi, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika pindi wanyamapori wanapoingia katika maeneo yao ya makazi.

d) Usafiri, Usafirishaji na Ujenzi

Vipindi vifupi vya mvua kubwa katika msimu huu vinaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara na reli, kuathiri shughuli za ujenzi na kusababisha kuongezeka kwa ajali katika sekta ya usafiri wa nchi kavu, kuchelewa na kuairishwa kwa safari za ndege, kwenye maji na reli, kukatika kwa mawasiliano katika shughuli za usafiri wa anga na kwenye maji, na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji katika shughuli za usafiri, usafirishaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa ujumla.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika kuzipata na kutumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu stamilivu pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

e) Nishati, Maji na Madini

Ongezeko la vina vya maji katika mabwawa na mito linatarajiwa kujitokeza hasa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani na hivyo kuongeza hatari ya mafuriko hususan katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko.

Kwa upande mwingine, kupungua kwa vina vya maji katika mabwawa na mitiririko ya mito kunatarajiwa kujitokeza katika maeneo ambayo mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa. Upungufu wa maji unaweza kupelekea ongezeko la gharama za kutibu maji kwa ajili ya majumbani. Matumizi endelevu ya rasilimali maji yanasisitizwa hasa katika umwagiliaji, uzalishaji wa umeme wa maji, shughuli za madini, matumizi ya viwandani na majumbani. Jamii na Mamlaka za Nishati na Maji zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuepuka athari zinazoweza kuathiri miundombinu ya maji na nishati.

f) Mamlaka za Miji na Wilaya

Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji, kuongeza mtiririko na kusababisha mafuriko ambayo yanaweza kupelekea uharibifu wa miundombinu na tishio la usalama wa maisha ya watu na mali. Mamlaka za miji zinashauriwa kuboresha na kuimarisha mifumo ya maji taka na safi mijini ili kupunguza athari za mafuriko. Jamii zinazoishi katika maeneo hatarishi zinashauriwa kuchukua hatua stahiki.

g) Sekta ya Afya

Hali ya maji kutuama inaweza kujitokeza na kutengeneza mazalia ya wadudu wadhurifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji kama vile mabwawa na visima vifupi. Pia, hali hii inaweza kusababisha milipuko ya magonjwa yanayohusiana na maji na wadudu wadhurifu. Hivyo, sekta husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba vya ziada katika vituo vya kutolea huduma za afya endapo itatokea miundombinu kuharibika. Pia, jamii inashauriwa kutibu maji ya kunywa, kuzuia na kuharibu mazalia ya mbu, kuzingatia matumizi sahihi ya vyoo, kuendeleza tabia ya kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kudumisha usafi wa mazingira. Aidha, kwa maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, jamii inaweza kulazimika kutumia maji yasiyo safi, ushauri unatolewa kwa wananchi kutibu maji kabla ya kuyatumia. Msisitizo unatolewa kwa mamlaka husika na jamii kwa ujumla kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari hasi zinazoweza kujitokeza.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

h) Sekta Binafsi

Shughuli za kilimobiashara na uzalishaji viwandani zinaweza kuathirika kutokana na upungufu wa malighafi za kilimo unaotokana na upungufu wa mvua hususan kwenye maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani. Hali hii, inaweza kusababisha ongezeko la gharama za upatikanaji wa malighafi na uendeshaji. Aidha, upungufu wa mvua unaweza kuathiri ubora wa bidhaa mfano miti ya nguzo, mbao, nyama na asali.

Wadau wa Sekta Binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

i) Menejimenti za Maafa

Katika msimu huu wa mvua, vipindi vya mvua kubwa vinaweza kutokea na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi ambayo yanaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu, mazingira, kupoteza mali na madhara kwa binadamu. Hivyo, Idara ya Usimamizi wa Maafa inashauriwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mipango, ambao utasaidia kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo, Idara ya Menejimenti ya Maafa nchini inashauriwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mipango itakayosaidia kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Wasimamizi wa shughuli za mazingira wanashauriwa kuzingatia taarifa hii ipasavyo. Aidha, sekta, mamlaka husika na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayohamasisha kuzuia au kupunguza madhara na kuhamasisha uhifadhi wa chakula.

j) Vyombo vya Habari

Waandishi wa Habari wanashauriwa kufuatilia na kupata taarifa sahihi za utabiri na tahadhari ya Hali ya hewa **kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)** na kuzisambaza kwa wakati ili kuelimisha umma na kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza. Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa wataalam ili kuandaa na kusambaza makala na ripoti za kisekta kwa lugha rahisi kwa lengo la kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu matumizi ya utabiri katika kukabiliana na athari za hali ya hewa.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa: 31 Oktoba, 2024

Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)